# Alichokiona Shangazi Sallie Kwenye Kikombe

## (What Aunt Sallie Saw In The Cup)

# Alichokiona Shangazi Sallie Kwenye Kikombe

## (What Aunt Sallie Saw In The Cup)

**na**

***"Wakristo wa Pacific"***

**Mai 1, 1912**

# Alichokiona Shangazi Sallie Kwenye Kikombe

## (What Aunt Sallie Saw In The Cup)

Toka ugunduzi wa uchafu, vijidudu, vibawasili, n.k., mababu wakuu wa mamgonjwa yote, tunashinikizwa kufuata sheria ya usafi wa hali ya juu sana. Maana Bwana mwema amejaza vyakula tunavyokula, maji tunayokunywa, na heawa hii tunayopumua, kwa haya madhara yanayouwa; ili kwamba kwa yule atakayeishi kwa muda mrefu kuvua viatu vyake, anapaswa kuchemsha maji anayokunywa, na kuchemsha mdomo na kila chakula atakachojaza mdomo wake, na anapaswa kuvaa sponchi puani, ili kumkinga na vijidudu hivi vinavyoua. Maana kifo hakina enzi, anayeshukuru yu karibu; agizo hilo limefungwa, makala haya yameendelea, na wote ambao hawaisujudii sura yake watatupwa wakiwa hai katika tundu la vijidudu.

Ama vyombo visafi vya kanisa uruhusiwa nay eye, maana katika kando ya kikombe ameanzisha enzi yake. Kutoka katika kinywa cha Ndugu Ayubu ilitokea ugonjwa wa mmeng'enyo wa chakula, Ndugu Adamu akaongeza nimonia, Ndugu Ibrahimu akachangia ugonjwa unaowavimbisha ng'ombe miguu, na Yuda akaweza kifua kikuu, na hivyo ivyo katika mzunguko huo. Hivyo kikombe kiliponifikia, ilionekana kama kifo katika usawa wake.

Hakika, nisingeweza kukishika; bali nilikipitisha kwa shangazi Sallie aliyezeeka, na kwa hakika jinsi niishivyo, alikigugumia, (sawa na kwamba alitaka kuchukua vya kutosha ili kusababisha kifo), na akakaa pale kimya, na akaonekana kama anafikiria kitu kingine. Na kweli niishivyo, bado yuko hai, na hiyo imekuwa zaidi ya mwaka mmoja; na hiyo si yote, anaifanya kila siku ya Bwana. (Ni siri kwangu.) Nadhani lazima **"atakuwa"** na magonjwa yote yanayosababishwa na vijidudu, na amekingwa na maradhi, sawa na kwamba unasurua. Lakini wangu! Siwezi kuihatarisha kwa ajili ya ulimwengu wote.

Kulikuwa na watu pale wakiwa na ndevu nyingi, ndevu nzuri kubwa, ambazo Bwana amesababisha zikue katika nyuso za wanaume kwa ajili yaa uendelevu na ugawaji wa vijidudu hivi, na wanakandamiza kikombe hiki vinywani mwao; na kizee shangazi Sallie anameza, na ikaonekana kufikiria kuhusu kitu kingine, nab ado anaishi. (Siwezi kuelewa.)

Sawa, nilikwenda kwa shangazi Sallie aliyezeeka, na nikamuuliza kama asingeweza kuona chochote katika kikombe kile; na kama

sijawahi kupata mshangao, ilikuwa ni kule. Alisema, “Ndiyo, mtoto, hakika, naweza. Kwa nini unaniuliza swali hilo?”

“Kwa nini…er…; nilidhani labda macho yako hayakuwa mazuri.”

Kwa nini, mtoto,”alisema, “Naweza kuona katika hicho kifo cha Bwana, na sihitaji miwani yangu iangalie hilo pia.”

Sawa, nilidhani nimeona kila aina ya kifo katika kikombe, lakini kuna moja ambayo sikuona wala kufikiria.

“*Maana kila muulapo mkate huu na kukinyweaa kikombe, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.*”

Imerudiwa kuchaapishwa kutoka ***“Wakristo wa Pacific”,*** Mai 1, 1912